

Jina _____

Hasira na Haki za Kibinafsi

Tarehe _____

Mtihani wa Toleo la 5

Darasa _____

_____ Gredi

Maswali ya Kweli au Sio Kweli (Alama 2 kwa kila swali)

Maagizo: Weka alama X iwapo jibu ni Sahihi.

Weka alama O iwapo jibu si Sahihi.

1. _____ Ikiwa utampa Mungu haki zako za kibinafsi, Mungu sasa anazimiliki – sasa ni haki za Mungu binafsi.
2. _____ Ikiwa mtu atampa Mungu haki zake za kibinafsi, anapaswa kumshukuru Mungu kwa kila jambo litakalotokea baadaye.
3. _____ Ikiwa mtu hampi Mungu haki zake za kibinafsi, na mtu akiuke (avunje, aende kinyume) na moja ya haki zake za kibinafsi) kwa kawaida atakasirikwa.
4. _____ Yesu alipokasirikwa, alitenda dhambi na ikabidi amuombe Mungu msamaha.
5. _____ Mungu hataki umpe haki zako za kibinafsi.
6. _____ Ikiwa mtu atampa Mungu haki zake za kibinafsi, kamwe Mungu hatamjaribu ili kuona kama amemaanisha.
7. _____ Wakristo wengi huwa wanafikiria jinsi ya kuonyesha upendo wao kwa Mungu wakati wanapomkasirikwa mtu mwingine.
8. _____ Ni vigumu sana kutenda dhambi wakati unapokuwa na hasira.
9. _____ Wakristo wengi huwa hawakasiriki baada ya kumpa Mungu haki zao za kibinafsi.
10. _____ Mungu ana sheria nyingi katika Biblia, ambazo zinakuelezea jinsi ya kujibu baada ya kumpa haki zako za kibinafsi.
11. _____ Machungu ya kale ambayo hayajatatuliwa yanaweza kuchochea shida yako ya hasira.
12. _____ Mtu anapokiuka moja kati ya haki ulizompa Mungu, unapaswa kila wakati kumjulisha kwamba amekosea kwa kufanya hivyo.

Maswali ya kuchagua jibu (alama 2 kwa kila swali)

Maagizo: Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi ya jibu lako katika mstari uliopo mbele ya swali.

1. _____ Mtu anapompa Mungu haki zake za kibinafsi, anapaswa:
 - A. Kukasirika kila wakati.
 - B. Kumkasirikia Mungu pekee yake.
 - C. Kumshukuru Mungu katika kile kitakachotendeka baadaye.

2. _____ Amri kuu katika Biblia inasema:
 - A. Mpende jirani yako.
 - B. Mpende Mungu.
 - C. Wapende Marafiki zako.

3. _____ Unapomkabidhi Mungu haki zako za kibinafsi, unapaswa:
 - A. Kujifunza kukuza maadili yatakayochukua nafasi ya haki hizo.
 - B. Kufunga na kuomba siku nzima kisha umwelezee mchungaji wako.
 - C. Kumuomba Mungu akurejeshee kama faida za ziada.

4. _____ Unazikabidhi haki zako za kibinafsi kwa Mungu kwa njia ya:
 - A. Kuwa Mkristo.
 - B. Kumwambia Mungu kwamba unataka awe mmiliki wa haki zako za kibinafsi.
 - C. Kuomba na kumtafuta wakili Mkristo.

5. _____ Majukumu yako binafsi ni:
 - A. Sawa na haki zako za kibinafsi.
 - B. Jambo ambalo ni haki yako kufanya.
 - C. Jambo ambalo umepewa ulifanye.

6. _____ Unapompa Mungu haki zako za kibinafsi Anaweza akakurujeshea baadhi yazo. Hizi hujulikana kama:
 - A. Haki za Kibinafsi.
 - B. Majukumu ya kibinafsi.
 - C. Marupurupu (faida za ziada).

Maswali ya Simulizi Fupi

1. Je, haki za kibinafsi ni zipi? Eleza maana ya maneno haya mawili “haki za kibinafsi”. (alama 5)

2. Kwa nini ni muhimu kumkapa Mungu haki zako za kibinafsi? (alama 5)

3. Elezea ni kwa njia ipi mtu anaweza kumpa Mungu haki zake za kibinafsi. (alama 8, 2 kwa kila swali)

1. _____

2. _____

3. _____

4. _____

4. A. Ni haki ipi moja yako ya kibinafsi ambayo imekiukwa ndani wiki chache zilizopita? (alama 4)

B. Ni sifa zipi njema za kindani hukusaidia zaidi kuitikia Kwa njia ya Mungu wakati haki hizi za kibinafsi zinapokiukwa? (alama 4)

C. Orodhesha mambo matatu unayoweza kuyafanya ili kukuza sifa hizi njema za kindani katika maisha yako. (alama 9, alama 3 kwa kila swali)

1. _____

2. _____

3. _____
